

## 1.5 Utawala

Halmashauri ya Pangani inaundwa na Tarafa 4, Kata 14, Vijiji 33 na vitongoji 96. Halmashauri hii kata zake zinapatikana katika maeneo mawili kwani kata 08 zinapatikana ng'ambo baada ya kuvuka mto Pangani na kata 06 zinapatika eneo la pili kabla ya kuvuka mto ukiwa unatokea Wilaya ya Tanga. Halmashauri hii ina Jimbo moja la Uchaguzi ambalo ni Jimbo la Pangani.

Halmashauri ina kamati za kudumu 5 kama ifuatavyo;

- ✓ Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango
- ✓ Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
- ✓ Kamati ya Elimu na Afya
- ✓ Kamati ya UKIMWI
- ✓ Kamati ya Maadili

Halmashauri ya Pangani ina jumla ya Divisheni 09 na Vitengo 09 katika ngazi ya juu kama ifuatavyo;-

***Divisheni za;***

1. Utawala na Usimamizi wa Rasilimiali Watu
2. Miundombinu, Maendeleo ya Vijiji na Mijini
3. Viwanda, Biashara na Uwekezaji
4. Elimu Sekondari
5. Afya Ustawi wa Jamii na Lishe
6. Mipango na Uratibu
7. Kilimo, Mifugo na Uvuvi
8. Maendeleo ya Jamii
9. Elimu ya Awali na Msingi

***Vitengo vya;***

1. Huduma za Sheria
2. Ukaguzi wa Ndani
3. Huduma za Ununuzi
4. Fedha na Hesabu
5. Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira
6. Teknolojia, Habari na Mawasiliano
7. Mawasiliano Serikalini
8. Udhhibiti wa Taka na Usafi wa Mazingira
9. Michezo, Utamaduni na Sanaa
10. Uchaguzi
11. Ufuatiliaji na Tathimini